

**Taarifa ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa [NIDA] kuhusu usajili wa Tanzania
waishio nje ya nchi [DIASPORA].**

**Mamlaka imemteua Bi. Rose Mdami [Mob. No: +255-713-412871] kuwa Afisa
Dawati atakayeshughulikia masuala ya Diaspora ndani ya Malaka ya NIDA.**

**Dawati hili litatoa huduma kwa haraka [Fast Track] kwa DIASPORA katika Jengo la
Magereza lililopo katika Barabara ya Kivukoni Mjini Dar es Salaam.**

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Bi. Mdami [Mob. No: +255-713-412871].

KITAMBULISHO CHA TAIFA NA FAIDA ZAKE KWA JAMII

Utangulizi - Kwa muda mrefu Tanzania imekuwa haina mfumo rasmi unaotambulika kumtambua mwananchi ambaye ni raia halisi wa Tanzania, mpaka Serikali ilipoamua kuanzisha daftari la kielektroniki lenye taarifa sahihi za watu kujibu maswali makuu manne:-

1. Nani ni nani?
2. Yuko wapi?
3. Anafanya nini?
4. Anamiliki nini?

Na matokeo ya kukamilika kwa mfumo huu wa utambuzi na usajili wa watu ni Kitambulisho cha Taifa

Faida za kukamilika kwa mfumo huu na kuanza kwa matumizi ya vitambulisho vya Taifa, zimegawanyika katika makundi makuu manne. Ulinzi na usalama wa nchi, kijamii, kisiasa na kiuchumi

- Vitambulisho vya Taifa, vitasaidia kuimarisha usalama wa raia na mali zao, na kupunguza vitendo vya uhalifu na hasa unaofanywa na raia kutoka nchi jirani na wafungwa waliomaliza adhabu zao au kuachiwa huru kwa msamaha wa Rais. Ni wazi kuwa udhibiti wao umekuwa mgumu kutopteka na kushindwa kuwatambua. Pia itasaidia kuweka kumbukumbu za matukio ya uhalifu katika daftari
- Vitambulisho vitasaidia kuboresha daftari la wapiga kura, na kuipunguzia mzigo mkubwa serikali katika kuboresha daftari hilo kila wakati uchaguzi unapowadnia
- Kutokana na Tanzania kuwa mwanachama katika Jumuia ya Afrika Mashariki, kitambulisho kitatumika kusafiria katy ya nchi wanachama wa Jumuiya, tofauti na sasa ambapo lazima msafiri kuwa na Hati ya kusafiria (PASSPORT)
- Vitambulisho vya Taifa vitasaidia kuwasajili na kuwatambua wananchi ambao watanufaika na upatikanaji wa ruzuku za pembejeo za kilimo na hivyo kufanikisha azma ya Kilimo Kwanza;
- Kitasaidia kumtambua mhusika anapohitaji kupatiwa huduma katika Taasisi mbalimbali kama vile; benki, Makampuni ya simu, Taasisi za mikopo, biashara, elimu, Polisi na Mahakama na huduma za afya n.k.
- Kitambulisho hiki kitasaidia serikali kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato na hivyo kuboresha huduma muhimu za kijamii kama vile; afya, elimu, barabara pamoja na ulinzi na usalama wa raia na mali zao;

- Kuweka kumbukumbu za matukio ya watu wote katika daftari la Utambuzi na usajili na hivyo kuisaidia Serikali na Taasisi binafsi katika shughuli za kila siku na katika kupanga vipaumbele;
- Wananchi kupata fursa ya kukopesheka kirahisi na kupata mitaji nafuu kutoka kwenye taasisi za kifedha na kupungua riba
- Kurahisisha Serikali kutoa fidia na msaada wa dharura wakati wa majanga
- Kusaidia kupunguza Wafanyakazi hewa kwenye Mfumo wa taarifa za Kiutumishi na Mishahara Serikalini; na

Kuhakikisha kuwa wananchi wanapata stahili zao za kijamii. Kwa mfano, kupata malipo ya pensheni, haki za matibabu, haki za kujunga na masomo ikiwa ni pamoja na stahili zozote ambazo zinahusu raia wa Tanzania ndani na nje ya Nchi

Mamlaka imechukua tahadhari zote katika kuhakikisha usalama na usiri wa taarifa unakuwepo katika ngazi na hatua zote za ukusanyaji, uchakataji na uhifadhi wa taarifa uliozingatia vigezo vyote kitaifa na kimataifa. Hii ni pamoja na kutunga kanuni na sheria kali zinazolinda na kudhibiti usalama na uhifadhi wa taarifa

Kitambulisho cha Taifa – Kimeanzishwa kwa lengo la kutambua na kuthibitisha uraia wa mtu; ili kumwezesha kupata haki zake zote msingi kama raia wa Tanzania kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kitambulisho cha Taifa ndio hati msingi inayotambulisha uraia wa mtu ndio maana kabla ya kupata kitambulisho cha Taifa lazima mwombaji kupita katika hatua zote zinazothibitisha uraia wake, uzaliwa wake na ukaazi wake. Na hili limekuwa likifanyika kwa kuhusisha wadau wote muhimu wenye dhamana kisheria ya kuthibitisha hayo mfano RITA, Uhamiaji, TAMISEMI n.k

NIDA inatoa vitambulisho vya aina tatu, kitambulisho cha Taifa kwa raia wa Tanzania, kitambulisho cha Taifa kwa wageni wakaazi (legal residents) na kitambulisho cha Taifa kwa wakimbizi. Kwa mujibu wa sheria ya uhamiaji; Tanzania ina raia aina tatu.

1. Raia kwa kuzaliwa
2. Raia kwa kurithi
3. Raia kwa kuandikishwa

Hivyo kutohana na matakwa ya sheria; vitambulisho kwa raia vitatolewa kwa raia waliopo katika makundi tajwa hapo juu. Wageni na wakimbizi wanaoishi kihalali nchini watapata vitambulisho vya Taifa kutegemeana na masharti na vibali vya kuishi nchini.